

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI / AGOSTI 2010
MUDA: SAA 2½

MTIHANI WA MUUNGANO WILAYA YA BUNGOMA 2010
Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI / AGOSTI 2010
MUDA: SAA 2½

MAAGIZO:

- Jibu maswali **manne pekee**
- Swali la kwanza ni la **lazima**
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Tamthilia, Riwaya, Hadithi Fupi na Ushairi.
- Usijibu maswali mawili kutoka katika sehemu moja.

SEHEMU YA A

sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.

Fasihi simulizi

1. a) Maghani ni nini? (alama2)
- b) Eleza fani zifuatazo za maghani. (alama8)
 - i) Vivugo
 - ii) Tondozi
 - iii) Pembezi
 - iv) Rara
- c) Eleza maana ya neno Ulumbi (alama2)
- d) Bainisha sifa za ulumbi. (alama8)

SEHEMU YA B

RIWAYA

UTENGANO – Said A. Mohamed

2. “Nyinyi mliosoma elimu yenu bure. Hamjui mnakotoka wala mnakokwenda...
Usinisemee kizungu miye. Si ndiyo mlivyotuweka tuisome tuwe wajinga...”
 - a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama4)
 - b) Itaje mbinu ya lugha iliyotumika hapa. (alama2)
 - c) Taja sifa za mzungumzaji. (alama4)
 - d) Kwa kujikita kwa wahusika wafuatao, jadili maudhui ya mabadiliko. (alama10)
 - i) Mussa
 - ii) Maksiudi
 - iii) Maimuna
 - iv) Farashuu
 - v) Biti Kocho
3. Dhihirisha uozo wa kijamii kama unavyojitokeza katika riwaya ya Utengano. (alama20)

SEHEMU YA C

TAMTHILIA

KIFO KISIMANI – K. wa Mberia

4. a) “Wewe ndiwe Butangi?”
“La! Lakini mimi ndiye kiongozi wa macho na masikio yake.”
“Na kisu chake cha kuchinjia watu.”
 - i) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)
 - ii) Ni ukinzani upi unaojitokeza katika dondoo hili? (alama6)
- b) Fafanua mbinu zifuatazo za lugha kama zilivyotumiwa na mwandishi wa tamthilia.

- i) Uzungumzi nafsia (alama4)
 ii) Lugha ya matusi (alama2)
 iii) Taswira (alama4)
5. a) Mwandishi anamsawiri mwanamke kama kiumbe aliyedhulumiwa. Jadili (alama10)
 b) Jadili maudhui ya tamaa kama yanavyojitokeza katika tamthilia (alama10)

SEHEMU YA D

HADITHI FUPI

MAYAI WAZIRI WA MARADHI – K. W. Wamitila

6. Eleza kwa kutumia mifano ifaayo vile ambavyo mwandishi wa hadithi ya **‘Uteuzi wa Moyoni’** amelishughulikia swala la jinsia na utamaduni (alama20)

SEHEMU YA E

USHAIRI

7. Soma shairi lifuatalo kwa makini halafu ujibu maswali yanayofuata.

- | | | | |
|----|--|-----|---|
| 1 | Kijana tuza makini, nikwambie usikile
Chakula mahotelini, si kizuri usikile
Ufikapo mlangoni, kizingiti usikile | 6. | Kileta maji jioni, ndoo jitwike na kata
Kata njema ya majani, laini wezayo kata
Kumbuka ya kisimani, huteki ela kwa kata |
| 2. | Nenda kaseme nyumbani, kesho asubuhi siji
Nitakwenda makondeni, kawashunge shunge siji
Na hata hapo jioni, kama nitakuja siji | 7. | Ninawahi kibandani, nikaliezeke paa
Nipate lindia nyuni, na wanyama kama paa
Kwani kiola angani, naona jua lapaa |
| 3. | Na kama wenda mjini, upatapo nyumba panga
Upahame mizimuni, palozingirwa na panga
Hapana tena amani, kutwa mwapigana panga | 8. | Kisha takwea mtini, nimeona bivu tunda
Sina usono moyoni, ela tunda kisha tunda
Nimpe wangu mwendeni, jioni nishike tunda |
| 4. | Na kesho kija shambani, uonapo mti panda
Kwea hadi kileleni, ujifiche kwenye panda
Kaziyo ulinde chini, mimea tuliyopanda | 9. | Meanza wao uneni, hapo nami ndipo kamba
Leo wenda hawaoni, kama wa bahari kamba
Wajijaza kimiani, wakijitatia kamba |
| 5. | Kishuka ola shinani, njugu merundika chungu
Njugu peleka nyumbani, zisije zikawa chungu
Kaanga sufuriani, au pia kwenye chungu | 10. | Mtoto wachoma yakini, japo liwe moja kaa
Ukikupata takoni, ni shida huwezi kaa
Ela hufaa mekoni, kutoka nswi na kaa |

Maswali.

- a) Bainisha dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama2)
- b) Eleza maana tatu za neno chungu kama lilivyotumika katika shairi (alama3)
- c) Andika ubeti wa nane katika lugha nathari (alama3)
- d) Eleza muundo wa shairi hili (alama5)
- e) Onyesha vile uhuru wa kishairi ulivyotumiwa na malenga (alama4)
- f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi (alama3)
 - i) Makondeni
 - ii) Jitwike
 - iii) Kiola